



## **MRADI WA KULETA MAGEUZI KATIKA SEKTA YA MKAA TANZANIA**

**KITINI CHA MAFUNZO KWA JAMII NGAZI  
YA KIJIJI KUHUSU UTAWALA BORA,  
JINSI NA JINSIA, NA UENDESHAJI WA  
SHUGHULI ZA SERIKALI**

Mafunzo haya yameandaliwa na Shirika la Kuhifadhi Misitu ya Asili Tanzania (TFCG) kwa ufadhili wa Shirika la Maendeleo na Ushirikiano la Uswisi (SDC)



Schweizerische Eidgenossenschaft  
Confédération suisse  
Confederazione Svizzera  
Confederaziun svizra

**July 2016**





# MRADI WA KULETA MAGEUZI KATIKA SEKTA YA MKAA TANZANIA

**KITINI CHA MAFUNZO KWA JAMII NGAZI  
YA KIJIJI KUHUSU UTAWALA BORA,  
JINSI NA JINSIA, NA UENDESHAJI WA  
SHUGHULI ZA SERIKALI**

Mafunzo haya yameandaliwa na Shirika la Kuhifadhi  
Misitu ya Asili Tanzania (TFCG) kwa ufadhili wa  
Shirika la Maendeleo na Ushirikiano la Uswisi (SDC)



Schweizerische Eidgenossenschaft  
Confédération suisse  
Confederazione Svizzera  
Confederaziun svizra

**July 2016**

# **YALIYOMO**

---

UTANGULIZI.....	3
<b>SEHEMU YA KWANZA .....</b>	<b>4</b>
<b>UTAWALA BORA.....</b>	<b>4</b>
1.2.1 Maana ya Utawala .....	4
1.2.2 Maana ya Utawala Bora.....	4
1.3.1 Demokrasia .....	4
1.3.2 Utawala wa Sheria.....	4
1.3.3 Haki na Usawa.....	4
1.3.4 Ushirikishwaji wa Wananchi .....	5
<b>SEHEMU YA PILI .....</b>	<b>6</b>
<b>UENDESHAJI WA SHUGHULI ZA SERIKALI.....</b>	<b>6</b>
2.1.1 Maana ya Kijiji .....	6
2.1.2 Mkutano Mkuu wa Kijiji .....	6
2.1.3 Majukumu na kazi za Mkutano Mkuu wa Kijiji .....	6
2.1.4 Halmashauri ya Kijiji.....	6
2.1.5 Kazi na wajibu wa Halmashauri ya Kijiji .....	7
2.1.6 Muundo wa Kamati za Halmashauri za Kijiji.....	7
2.1.7 Majukumu na kazi za kamati za Halmashauri za Kijiji .....	7
2.1.8 Majukumu ya Mwenyekiti wa Kijiji.....	9
2.1.9 Majukumu ya Afisa Mtendaji wa Kijiji .....	9
2.2.10 Maana ya Kitongoji.....	9
2.2.11 Mkutano wa wakazi wa Kitongoji .....	9
2.2.12 Kazi za mwenyekiti wa Kitongoji.....	10
<b>SEHEMU YA TATU .....</b>	<b>14</b>
<b>JINSI NA JINSIA.....</b>	<b>14</b>
3.5 Jinsi ya kuweka usawa wa kijinsia katika ngazi ya Kijiji .....	19

## UTANGULIZI

---

Mafunzo haya yameandaliwa na kuletwa kwenu na Shirika la Kuhifadhi Misitu ya Asili Tanzania (TFCG) kwa ufadhili wa Umoja wa Ulaya (*European Union*) kuitia Mradi wa Utekelezaji wa Mbinu mbalimbali za kukabiliana na Mabadiliko ya Tabia nchi katika milima ya Usambara Mashariki, Wilaya ya Muheza Mkoa wa Tanga.

Lengo kuu la mafunzo haya ni kuwajengeta uwezo viongozi katika ngazi ya kijiji na jamii kwa ujumla kuhusu dhana nzima ya utawala na misingi ya utawala bora; Jinsia; na utaratibu wa uendeshaji wa shughuli za serikali katika ngazi ya kijiji. Mafunzo haya ni muhimu sana kwani yatawapatia elimu itakayowasaidia katika kufanya maamuzi sahihi ya kupata viongozi sahihi katika ngazi mbalimbali za uongozi ngazi ya kijiji, watakaofanya kazi kwa kuzingatia misingi ya utawala bora, jinsia na utaratibu uliowekwa na serikali wa kuendesha shughuli za serikali kwa ajili ya maendeleo endelevu ya wananchi wote.

Kupitia Mradi wa Utekelezaji wa Mbinu mbalimbali za kukabiliana na Mabadiliko ya Tabia nchi katika milima ya Usambara Mashariki; vikundi mbalimbali vitaanzishwa hapa kijijini na uanzishwaji wake ni lazima uzingatia utaratibu uliowekwa na serikali wa uendeshaji wa shughuli za serikali, jinsia na misingi ya utawala bora. Rai yetu ni kuwaomba viongozi wa kijiji na jamii kwa ujumla kuupokea mradi huu na kuutekeleza kwa kuzingatia misingi hiyo iliyowekwa na serikali kwa manufaa yetu wote. Mafunzo haya yatawaongezea uwezo zaidi wa kutambua misingi iliyowekwa na serikali kuhusu jinsia, utawala bora na jinsi ambavyo viongozi wetu wanapaswa kutekeleza shughuli za serikali ngazi ya kijiji.

Mabadiliko ya tabia nchi ni suala mtambuka. Madhara yake yameonekana duniani kote na sasa imekuwa ni kilio cha watu wengi, huku waathirika wakubwa zaidi wakiwa ni wakulima. Wananchi wa Usambara Mashariki na hasa wale wanaoishi katika Kata ya Misalai na Zirai naweza kusema wanayo bahati ya kipekee kabisa ya kufikiwa na mradi huu. Tunatoa rai waupokee mradi huu kwa mikono miwili na wautekeleze kwa moyo mmoja kwani kufanikiwa kwake ndio suluhisho la kudumu la matatizo mengi yanayowakabili hasa yale yanayohusiana na mabadiliko ya tabia nchi.

Wakati sasa umefika (kupitia mafunzo haya) wa kutimiza dhana ya utawala bora na jinsia kwa vitendo. Utawala bora unaozingatia jinsia katika kutekeleza shughuli za serikali ngazi ya kijiji; shughuli za kuhifadhi rasilimali za Misitu katika misingi endelevu; kusimamia utekelezaji wa mpango wa matumizi bora ya ardhi; kuhifadhi vyanzo vya maji na kusimamia matumizi endelevu ya maji; kutekeleza mbinu za kilimo bora tena chenye uwezo wa kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi; kusimamia uanzishwaji na uendelezwaji wa vikundi mbalimbali vya jamii kwa ajili ya kujiongezea kipato n.k.

Tunawatachia mafanikio mema katika mafunzo haya na katika kutekeleza mradi huu. Mafanikio mema katika uongozi na utekelezaji wa shughuli mbalimbali za serikali katika ngazi ya kijiji.

# SEHEMU YA KWANZA

## UTAWALA BORA

<b>Lengo la Somo</b>	Kuelimisha viongozi katika ngazi ya kijiji na jamii kwa ujumla kuhusu dhana nzima ya utawala na misingi ya utawala bora. Elimu itakayowasaidia katika kufanya maamuzi sahihi ya kupata viongozi sahihi watakaofanya kazi kwa kuzingatia misingi ya utawala bora kwa ajili ya maendeleo endelevu ya wananchi wote.
----------------------	---

### 1.1 Utangulizi

Ngazi ya Kijiji, Kitongoji na Mtaa ndiyo kitovu cha demokrasia shirikishi hapa nchini; hapa ndipo mwanzo wa Serikali ambapo kila mkazi wa Kijiji, Kitongoji na Mtaa anaweza kuhudhuria na kushiriki kikamilifu katika maamuzi yanayohusu ustawi na maendeleo yake mwenyewe na ya eneo anamoishi.

### 1.2 Maana ya Utawala na Utawala Bora

#### 1.2.1 Maana ya Utawala

Ni mchakato wa kufanya maamuzi na namna ambayo maamuzi yanatekelezwa au hayatekelezwi.

#### 1.2.2 Maana ya Utawala Bora

Utawala Bora ni utaratibu wa utumiaji wa madaraka ya umma kusimamia raslimali ya nchi katika jitihada ya kuongeza na kutumia raslimali hiyo kwa ajili ya kuinua hali ya maisha ya wananchi. Utumiaji huo wa madaraka huandamana na ushirikishaji wa wahusika wote katika kuhakikisha kuwa shughuli za umma zinaendeshwa kwa kuzingatia mawazo na maslahi ya wengi, utawala wa sheria, ushirikishwaji wa wananchi, haki, usawa, uwazi na uwajibikaji.

### 1.3 Misingi ya Utawala Bora

#### 1.3.1 Demokrasia

Demokrasia ni utaratibu ambamo viongozi wa wananchi hupatikana kwa njia ya uchaguzi unaoendeshwa kwa njia ya haki inayompa mwananchi uhuru wa kuchagua kiongozi anayemtaka. Miongoni mwa taratibu zinazopaswa kufuatwa katika kudumisha demokrasia ya kweli ni pamoja na watu kujijengea utamaduni wa:

- Uvumilivu na staha kwa mitazamo na maoni tofauti ya kisiasa;
- Kufuata na kuheshimu mawazo ya walio wengi;
- Kutumia nguvu ya hoja na siyo hoja ya nguvu;
- Kupingana bila kupigana; na
- Kujikosoa na kukosoana bila kuleana.

#### 1.3.2 Utawala wa Sheria

Katika utawala wa sheria kila mtu anapaswa kuzingatia na kuongozwa na Katiba ya Nchi, Sheria, Kanuni na taratibu zilizopo katika maisha yake mwenyewe, katika uhusiano na wengine na katika utekelezaji wa majukumu yake. Kiongozi hatarajiwi kupuuza au kujiweka juu ya sheria, maamuzi au maelekezo halali yaliyopo au kufanya kitendo chochote kinyume cha Katiba ama nje ya sheria. Matendo kama hayo ni batili na yanaweza kumfanya mhusika kuchukuliwa hatua za kisheria.

#### 1.3.3 Haki na Usawa

Kiongozi anatakiwa kufanya maamuzi na kutekeleza majukumu yake kwa kuzingatia haki bila ubaguzi wala upendeleo wa aina yoyote ile. Kwa kufanya hivyo kiongozi atajenga moyo wa imani kwa wananchi na itakuwa rahisi zaidi kwake kupata ushirikiano wao katika harakati za maendeleo na pia katika vita dhidi ya umaskini. Ni muhimu sana kwa kiongozi kuhakikisha kuwa haki za akina mama, watoto, wazee, na wasiojiweza zinazingatiwa na kulindwa wakati wote.

#### **1.3.4 Ushirikishwaji wa Wananchi**

Maendeleo endelevu ya watu huleta na watu wenyewe na wala hayaletwi na viongozi wala wafadhili. Viongozi wanatakiwa wawashirikishe wananchi katika maamuzi yote yanayohusu ustawi na maendeleo yao. Viongozi watatekeleza jukumu hili kwa kuitisha mikutano ya wakazi wote wa mitaa, vijiji na vitongoji kama inavyoelekezwa katika sheria, kanuni na miongozo iliyopo, yaani:

- Mkutano wa Wakazi wote wa mtaa mara moja kila baada ya miezi miwili;
- Mkutano wa wakazi wote wa kitongoji, mara moja kila mwezi; na
- Mkutano wa wakazi wote wa kijiji mara moja kila baada ya miezi mitatu.

#### **1.3.5 Uwajibikaji na Uwazi**

Viongozi pamoja na watumishi wa Halmashauri katika ngazi zote wapo kuwashudumia wananchi na sio kuwatawala au kuwaburuza. Viongozi wanaochaguliwa na wananchi wanatarajiwa kuwa karibu na wananchi wakati wote na wanapaswa kutoa taarifa za mara kwa mara kuhusu maamuzi pamoja na utendaji wao. Taarifa hizo zitawawezesha wananchi kupima na kuamua kama wanatekeleza wajibu wao kadri inavyotakiwa au la. Hali kadhalika, maamuzi na vitendo vyote vya viongozi katika utekelezaji wa majukumu yao lazima vifanywe bila kificho iii wananchi watambue kinachoendelea.

### **1.4 Wajibu wa Wananchi na Viongozi katika mfumo wa Demokrasia ya Vyama vingi vya Siasa**

#### **1.4.1 Wajibu wa wananchi:**

Wajibu wa wananchi ni pamoja na:

- Kushiriki kwa ukamilifu katika shughuli za kiuchumi na kijamii;
- Kushiriki kwa ukamilifu katika shughuli za siasa kama vile kugombea au kupigia kura wagombea mbalimbali;
- Kujielimisha juu ya sheria, kanuni na taratibu mbalimbali na matakwa ya Katiba kuhusu maendeleo ya siasa katika maeneo yao iii waweze kutumia haki yao kwa busara na kumchagua mgombea ye yote wampendaye;
- Kujenga na kulinda amani, mshikamano na maelewano kati yao.

#### **1.4.2 Wajibu wa Kiongozi:**

Wajibu wa kila Kiongozi wa Serikali wa kuchaguliwa katika ngazi ya Kijiji, Kitongoji au Mtaa ni pamoja na:

- Kutambua na kuzingatia kuwa mfumo wa vyama vingi ni mfumo wa ushindani wa ufanisi katika kuwashudumia wananchi na wala si uhasama hata kidogo;
- Kujua na kutambua vyote vya Siasa vilivymo katika himaya yake;
- Kuhakikisha kuwa shughuli za Serikali za Mitaa zinaendeshwa kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu zake na kwamba vyama vyote vya siasa vinazitekeleza ipasavyo;

### **1.5 Sifa za Kiongozi Bora**

Ili kuwa na utawala bora ni lazima kuwa na viongozi bora. Kiongozi bora anatakiwa kuwa na sifa zifuatazo:

- Awe mwezeshaji anayetumia mbinu za upangaji wa mipango shirikishi
- Awe na uwezo wa kusimamia utekelezaji wa sheria, kanuni na taratibu bila upendeleo wa aina yoyote;
- Anahakikisha kwamba huduma zinatolewa kwa haki na usawa bila kujali imani na itikadi za watu katika eneo lake;
- Anashiriki kwa ukamilifu katika harakati za kuondoa umaskini na kupiga vita rushwa;
- Anahakikisha kuwa uongozi na utawala katika Kijiji, Kitongoji au Mtaa wake unalingana na dhana na misingi ya utawala bora na demokrasia.

### **1.6 Hitimisho**

Mada hii imeelezea maana / dhana ya utawala bora na misingi yake. Aidha, mada hii imeainisha wajibu wa wananchi na Kiongozi wa Serikali wa kuchaguliwa katika ngazi ya Kijiji, Kitongoji na Mtaa. Kila kiongozi wa Serikali wa kuchaguliwa katika ngazi ya Kijiji, Kitongoji na Mtaa anapaswa kuhakikisha kwamba uongozi na utawala wa eneo lake unafuata misingi ya utawala bora na kwamba mwenendo wake unalingana na sifa za kiongozi bora wa kuchaguliwa zilizoainishwa katika mada hii.

# SEHEMU YA PILI

## UENDESHAJI WA SHUGHULI ZA SERIKALI

<b>Lengo la Somo</b>	Kuelimisha viongozi na jamii kwa ujumla kuhusu utaratibu wa uendeshaji wa shughuli za serikali katika ngazi ya kijiji. Wafahamu wajibu na majukumu ya kila kiongozi katika ngazi mbalimbali za uongozi. Kuwawezesha wananchi kuhoji na kupata majibu sahihi kwa lengo la kuongeza uwajibikaji na ufanisi wa viongozi waliowaweka madarakani katika nafasi mbalimbali za uongozi katika ngazi ya kijiji.
----------------------	---

### 2.1 Ngazi ya Kijiji

#### 2.1.1 Maana ya Kijiji

Kijiji ni eneo katika Tanzania Bara liloandikishwa kama kijiji likiwa na kaya sizizopungua 250 kwa mujibu wa Sheria ya Serikali za Mitaa inayohusu Mamlaka ya Wilaya

#### 2.1.2 Mkutano Mkuu wa Kijiji

Mkutano Mkuu wa Kijiji unajumuisha wakazi wote wa kijiji wenye umri kuanzia miaka 18. Kazi za mkutano mkuu ni kuchagua Mwenyekiti na wajumbe wa Halmashauri ya Kijiji na kuwaondoa wajumbe isipokuwa Mwenyekiti atakayeondolewa kulingana na taratibu zinazotolewa na waziri. Mkutano Mkuu wa kijiji huitishwa;

- Mara moja kila baada ya miaka mitano kumchagua mwenyekiti na wajumbe wa Halmashauri ya Kijiji au kila uchaguzi unapoitishwa
- Kila baada ya miezi mitatu kujadili ustawi na maendeleo ya Kijiji
- Wakati wowote kila jambo ambalo ni la muhimu kwa wakazi wa Kijiji linapojitokeza

#### 2.1.3 Majukumu na kazi za Mkutano Mkuu wa Kijiji

Majukumu ya mkutano mkuu wa kijiji ni kama ifuatavyo

- Kupokea na kujadili taarifa za utekelezaji wa shughuli za maendeleo ya kijiji iliyowasilishwa na Halmashauri ya kijiji
- Kupokea na kujadili taarifa ya mapato na matumizi ya fedha za Kijiji tangu Mkutano uliopita.
- Kupokea na kujadili taarifa ya makusanyo ya mapato ya kijiji
- Kupokea na kujadili mapendekezo yatakayotolewa na Serikali ya kijiji kuhusu kutunga sheria ndogo kwa manufaa ya kijiji
- Kupokea na kujadili taarifa za watu waliomba ardhi na kupewa au kunyimwa ardhi katika kijiji
- Kuzungumzia mambo mengine yanayohusu maendeleo ya Kijiji
- Kupokea maelekezo yalitolewa ngazi za juu za Serikali na kuweka mikakati ya kuyatekeleza

#### 2.1.4 Halmashauri ya Kijiji

##### Muundo wa Halmashauri ya Kijiji

Halmashauri ya Kijiji huundwa na kijiji kilichopewa usajili kwa mujibu wa sheria za Serikali za mitaa ikiwa na wajumbe wasiopungua 15 na wasiozidi 25 kama ifuatavyo

- Mwenyekit ambaye huchaguliwa na Mkutano Mkuu wa Kijiji
- Wenyeviti wa vitongoji vilivyoko kwenye Kijiji
- Wajumbe wengine wanaochaguliwa na Mkutano Mkuu wa Kijiji amba robo yake lazima wawe ni wajumbe wanawake.

Afisa Mtendaji wa Kijiji ndio Katibu wa Halmashauri ya Kijiji. Halmashauri ya Kijiji inakuwa inakutana kila mwezi lakini mwenyekiti wa Kijiji anaweza kuitisha kikao cha Halmashauri ya Kijiji wakati wowote kama anaona inafaa.

## **2.1.5 Kazi na wajibu wa Halmashauri ya Kijiji**

Yafuatayo ni baadhi ya majukumu ya Halmashauri ya Kijiji

- a. Kuhakikisha kuwa kuna ulinzi na usalama Kijijini
- b. Kupokea na kujadili taarifa za Kamati mbalimbali Kijijini
- c. Kupokea na kujadili maombi ya watu wanaohitaji ardhi Kijijini
- d. Kusimamia maendeleo ya kiuchumi na kijamii Kijijini
- e. Kupokea na kujadili taarifa za mapato na matumizi ya Kijiji
- f. Kupokea na kujadili taarifa za mambo yaliyotokea katika ngazi ya vitongoji
- g. Kupokea maelekezo kutoka Kamati ya Maendeleo ya Kata na Halmashauri ya Wilaya
- h. Kutunga sheria ndogo kwa manufaa ya Kijiji kulingana na taratibu zilizowekwa
- i. Kuwa wakala wa Serikali Kuu, Halmashauri ya Wilaya na Mji kama itakavyoafikiwa kati ya Halmashauri ya Kijiji na mamlaka husika
- j. Kufanya mambo yoyote kama itakavyoolekezwa na Mkutano Mkuu wa Kijiji

## **2.1.6 Muundo wa Kamati za Halmashauri za Kijiji**

Ili kutekeleza shughuli zake kwa ufanisi kamati za Halmashauri ya Kijiji zinaudwa na

- a. Kamati ya Fedha, Uchumi na Mipango
- b. Kamati ya Huduma za Jamii na Shughuli za Kujitegemea
- c. Kamati ya Ulinzi na Usalama

## **2.1.7 Majukumu na kazi za kamati za Halmashauri za Kijiji**

### **2.1.7.1 Kamati ya Fedha, Uchumi na Mipango**

- a. Kubuni miradi mbalimbali ya maendeleo ya Kijiji
- b. Kuunganisha mipango yote inayotokana na kamati nyingine Kijijini na ile ya Kiwilaya na Kitaifa inayotekelawa Kijijini
- c. Kupanga makadirio ya mapato na matumizi kwa shughuli zinazotakiwa kufanyika Kijijini
- d. Kuweka hesabu zote sahihi za shughuli zote Kijijini na kuhakikisha kuwa fedha zote zinatumika kama ilivyokusudiwa na zile ambazo hazijatumika zinawekwa kwenye akaunti ya Kijiji
- e. Kusimamia ukusanyaji wa mapato Kijijini
- f. Kuhakikisha kuwa kanuni zote za kilimo bora zinafuatwa Kijijini yaani:
  - Kutayarisha mashamba mapema;
  - Kuchagua mbegu bora na zenye uwezo wa kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi,
  - Kuweka mbolea ya kupandia na kukuzia mashambani;
  - Kupanda mapema kwa kufuata mazingira na hali ya hewa;
  - Kuhimiza kilimo cha makinga maji na kilimo msitu.
  - Kuhifadhi mazao ghalani;
  - Kusafisha mashamba baada ya mavuno;
  - Uvuvi bora unaohakikisha hifadhi ya mazalio ya samaki na mazingira.
- g. Kuhakikisha kuwa kila mwananchi anashiriki katika shughuli za kupiga vita umaskini
- h. Kutafuta njia za kukuza mapato ya Kijiji kwa maendeleo ya Kijiji

### **2.1.7.2 Kamati ya Ulinzi na Usalama**

- a. Kuhakikisha kuwa mikakati ya ulinzi na usalama inawekwa ili kulinda jamii na mali zake
- b. Kuhakikisha kuwa mafunzo ya mgambo na sungusungu yanafanyika na kuwa sungusungu na mgambo wanaendesha shughuli za ulinzi na usalama
- c. Kushirikiana na Kamanda wa Ulinzi na Usalama wa Wilaya kupeana taarifa za uharifu na nyingine zenye manufaa kwa usalama wa Taifa
- d. Kuhakikisha kuwa hakuna biashara ya magendo inayofanyika Kijijini
- e. Kudhibiti biashara na matumizi ya madawa ya kulevyia Kijijini ikiwa ni pamoja na kudhiti kilimo cha bangi na mirungi
- f. Kusimamia utekelezaji wa Sheria ndogo za Kijiji na Sheria za Serikali za Mitaa kwa ujumla

### **2.1.7.3 Kamati ya Huduma za Jamii na Shughuli za Kujitegemea**

#### **Majukumu ya Jumla**

- a. Kuhakikisha kuwa watoto waliofikia umri wa kwenda shule wanaandikishwa na kuhuduria masomo mpaka wanamaliza elimu ya msingi
- b. Kuhamasasisha ujenzi na ukarabati wa majengo na miundombinu ya shule, zahanati, masoko, machinjio, majosho nakadhalika na kuwashirikisha watalaamu wanaojihusisha na mambo hayo
- c. Kuhamasishwa wananchi wote kuhuduria mikutano yote Kijiji iliyoitishwa kwa mujibu wa sheria
- d. Kuweka taratibu za utekelezaji wa shughuli za kujitegemea
- e. Kuhamasisha wananchi kuhuduria sherehe za kitaifa na mikutano ya hadhara inayoitishwa na Serikali, Halmashauri, Mbunge na Diwani
- f. Kuhamasisha jamii kuchukua hatua stahiki ili kujikinga na magonjwa na pia kuimarisha afya ya jamii
- g. Kuhakikisha kuwa shughuli za usimamizi na uhifadhi wa mazingira zinatekelezwa ili kuepukwa majanga yatokanayo na uharibifu wa mazingira

#### **Majukumu ya kiafya;**

- a. Kusimamia utekelezaji wa masharti ya kuzuia mlipuko wa magonjwa pamoja na masharti ya kuweka mazingira ya kijiji katika hali ya usafi
- b. Kuchukua hatua za kubaini magonjwa sugu kijiji na kuchukua hatua za kujenga zahanati/ kliniki kama huduma kwa wakazi.
- c. Kuchukua hatua za kinga kuzuia maradhi hasa UKIMWI na kutoa ushauri wa watu ambaa wameathirika na ugonjwa huu wa hatari.
- d. Kuweka mazingira ya kijiji katika hali ya usafi
- e. Kuchukua hatua za kutunza mazingira ili kuboresha afya
- f. Kuchukua hatua za kuboresha tija ya chakula na kutumia vyakula vyenye lishe ili kuboresha afya ya watu wazima na watoto.
- g. Kuchukua hatua za kuhimiza usafi wa mwili na mavazi kwa wanakijiji
- h. Kuchukua hatua za kuelimisha na kuhimiza uzazi wa mpango kwa wanakijiji.
- i. Kuchukua hatua nyingine zozote za kuboresha afya kijiji kwa kuzingatia mazingira na haja za wakati.

#### **Majukumu ya Kiujenzi na Miundombinu**

- a. Kushughulikia ujenzi wa nyumba bora
- b. Kuwaelimisha na kuwashirikisha wanakijiji katika ujenzi wa nyumba bora
- c. Kusaidia kutafuta vifaa vya ujenzi
- d. Kujenga mabwawa/visima kufuatana na uwezo na mahitaji ya wanakijiji
- e. Kubuni mikakati na mbinu za ujenzi wa nyumba na majumba kijiji
- f. Kutatuta ufundi mbalimbali wa viwanda vidogovidogo
- g. Kuona kuwa nyumba za wanakijiji zinajengwa mahali pazuri, mathalani pasipoweza kuathiriwa na mafurikao, upopo mkali, vumbi na kadhalika
- h. Kuona kuwa nyumba zinajengwa kwa kuzingatia kanuni za afya
- i. Kutayarisha makisio ya kupata fedha za kupeleka katika Kamati ya Mipango na fedha ili kujadiliwa.
- j. Kuweka kumbukumbu ya wanakijiji wenye ujuzi wa kujenga, mfano waseremala, mafundi uashi na kadhalika na kuwashirikisha katika kazi za ujenzi kijiji.
- k. Kutafuta mipango mbalimbali ya usafiri na uchukuzi wa mazao na bidhaa zinazoingia au kutoka kijiji
- l. Kushirikiana na vijiji vingine vya jirani ili kuanzisha ushirika wa aina mbalimbali, mfano

- uchukuzi, kuchimba visima na kadhalika
- m. Kuhakikisha kuwa barabara zinazounganisha kijiji na vijiji jirani zinapitika wakati wote
  - n. Kuwashirikisha wanakijiji katika ujenzi na ukarabati wa barabara.

Kamati zote za Kudumu za Kijiji zinatakiwa kukutana kabla ya mukutano wa Halmashauri ya Kijiji na zitawajibika kutoa taarifa kwenye mukutano wa Halmashauri ya Kijiji.

### **2.1.8 Majukumu ya Mwenyekiti wa Kijiji**

Yafuatayo ni baadhi ya Majukumu ya Mwenyekiti wa Kijiji

- a. Atakuwa ndiye mkuu wa Serikali ya Kijiji
- b. Atakuwa na wajibu wa kuitisha na kuongoza mikutano ya Halmashauri ya Kijiji pamoja na Mikutano Mikuu ya Kijiji. Iwapo Mwenyekiti hatakuwepo basi wajumbe wa Halmashauri ya Kijiji wanaweza kuchagua mjambe yejote awe Mwenyekiti wa mukutano
- c. Atakuwa mwakilishi wa Kijiji kwenye Kamati ya Maendeleo ya Kata
- d. Atawahudumia wananchi wote kwa usawa bila kujali tofauti za kinjinsia, kisiasa, kidini na kimaumbile
- e. Atakuwa mfano wa uongozi bora na utendaji kwa kuwa na shughuli za kujitegemea ambazo zinaweza kuingwa na wanakijiji wenzake

### **2.1.9 Majukumu ya Afisa Mtendaji wa Kijiji**

Afisa Mtendaji wa Kijiji ni mtumishi wa Halmashauri ya Wilaya, Mji, Manispaa au Jiji na anawajibika kwa Halmashauri ya Kijiji katika utendaji kazi wake.

#### **Majukumu ya Afisa Mtendaji wa Kijiji:**

- a. Atakuwa ndiye mtendaji mkuu wa shughuli zote za kijiji
- b. Atakuwa ndiye mwandishi na mtunzaji wa kumbukumbu zote za vikao vyta kijiji, pamoja na rejestra ya kijiji na nyaraka nyingine muhimu za kijiji ikiwa ni pamoja na hati ya kuandikishwa kijiji
- c. Atakuwa ni mshauri mkuu kijijini katika kubuni na kutekeleza miradi ya maendeleo kijijini
- d. Atakuwa msimamizi mkuu wa utekelezaji wa miradi yote iliyobuniwa na Serikali ya Kijiji, pamoja na miradi mingine ya Serikali inayotekeliza katika eneo la kijiji
- e. Ataratibu shughuli za maofisa wa kiseka kijijini
- f. Atawajibika kuwasilisha taarifa muhimu za kijiji chake kwa Afisa Mtendaji wa Kata

## **2.2 Ngazi ya Kitongoji**

### **2.2.10 Maana ya Kitongoji**

Kitongoji ni sehemu ya Kijiji, Mamlaka ya Mji Mdogo au Mamlaka ya Mji. Eneo la Kijiji linatakiwa kugawanywa katika vitongoji visivyozi vitano kulingana na idadi ya kaya na jiografia ya eneo husika.

### **2.2.11 Mkutano wa wakazi wa Kitongoji**

Mkutano wa wakazi wa Kitongoji unahudhuriwa na wakazi wa Kitongoji wenye umri wa kuanzia miaka 18 na kuendelea. Mkutano wa Kitongoji una mamlaka ya kumchagua na kumwondo Mwenyekiti wa Kitongoji. Mkutano wa Kitongoji hufanya mara moja kila mwezi ili kujadili ustawi na maendeleo ya Kitongoji. Ila unaweza kuitishwa na Mwenyekiti wa Kitongoji wakati wowote jinsi atakavyoona inafaa na pindi jambo la dharula lenye manufaa ya kipekee kwa wanakitongoji.

### **2.2.11.4 Kazi na Majukumu ya Mkutano wa wakazi wa Kitongoji**

Mbali na mambo mengine mkutano wa wakazi wa Kitongoji utakuwa na majukumu yafuatayo.

- a. Kupokea na kujadili taarifa za utekelezaji wa shughuli za maendeleo ya Kitongoji kama zitakavyowasilishwa na Mwenyekiti wa Kitongoji
- b. Kujadili taarifa za utekelezaji wa mikakati ya kupambana na umaskini
- c. Kujadili hali ya ulinzi na usalama na maendeleo katika kitongoji
- d. Kuweka mikakati ya kupambana na ugonjwa wa UKIMWI

- e. Kupokea maelekezo kutoka Halmashauri ya Kijiji na kuweka mikakati ya utekelezaji wake katika Kitongoji

### **2.2.12 Kazi za mwenyekiti wa Kitongoji**

#### **Kazi za Mwenyekiti wa Kitongoji**

Mwenyekiti wa Kitongoji atakuwa na kazi zifuatazo;

- a. Kuitunza rejestra ya wakazi wa kitongoji na habari nyingine muhimu zinazohusu maendeleo ya kitongoji kwa jumla ikiwa ni pamoja na kumbukumbu za vizazi na vifo.
- b. Kusimamia shughuli za ulinzi na usalama wa watu na mali zao waishio katika eneo lote la kitongoji .
- c. Kuhamasisha ulipaji wa kodi na ushuru mbalimbali, kama utakavyoamuliwa na kuwekwa mara kwa mara na Halmashauri ya Wilaya, Mji, Manispaa au Jiji.
- d. Kusimamia katika eneo lake suala zima la Hifadhi ya Mazingira hususan vyanzo vyaa maji, Misitu n.k.
- e. Kusimamia suala la afya katika eneo lake ikiwa ni pamoja na utekelezaji wa kampeni za afya za Kitaifa, kimkoau kiwilaya dhidi ya magonjwa ya kuambukiza, na hasa vita dhidi ya UKIMWI.
- f. Kusimamia utekelezaji wa kanuni za kilimo na ufugaji bora iii kuinua hali ya lishe na uchumi wa wakazi wa kitongoji
- g. Kufuatilia na kuhakikisha kuwa kila mtoto mwenye umri wa kwenda shule anapatiwa nafasi na kushirikiana na viongozi wa shule katika kudhibiti utoro shulenii
- h. Kuhamasisha elimu ya watu wazima
- i. Kusimamia na kuwahamasisha wakazi wa kitongoji katika kutekeleza shughuli za kujitegemea
- j. Kusuluuhisha migogoro midogo midogo isiyostahili kushughulikiwa na Mabaraza ya Kata au mahakama
- k. Kuwakilisha kitongoji katika Serikali ya Kijiji.
- l. Kuwaongoza na kuwahamasisha wakazi wa kitongoji washiriki katika sherehe za Taifa na mikutano ya hadhara itakayoandaliwa na kuitwa na Serikali au Halmashauri.
- m. Kutekeleza kazi nyingine atakazopangiwa na Halmashauri ya Kijiji, Wilaya, Mji, Manispaa au Jiji.
- n. Mwenyekiti anaweza kuteua Kamati ya Ushauri yenyewajumbe wasiozidi watatu ambaa ni wakazi wa kitongoji hicho kwa ajili ya kushauri juu ya mambo mbalimbali yenyewmaslahi kwa kitongoji kinachohusika

### **2.3 Kamati ya Maliasili ya Kijiji**

#### ***Maana yake***

Kamati ya maliasili ya kijiji ni kamati inayochaguliwa na mkutano mkuu wa kijiji husika kwa ajili ya kusimamia zoezi la usimamizi shirikishi wa misitu kwa niaba ya kijiji. Kamati hii ni kamati ndogo ndani ya Kamati ya Huduma za Jamii na Shughuli za Kujitegemea.

#### **2.3.1 Sifa za Kamati**

Sifa zifuatazo ni muhimu kwa Kamati ya maliasili ya kijiji;

- i. Kamati inatakiwa kuwa na wajumbe wasiopungua 12
- ii. Wajumbe wawe wanajua kusoma na kuandika
- iii. Wajumbe wawe wanaujua vizuri msitu na matumizi yake
- iv. Wajumbe wawe wanatoka katika kila kitongoji na hasa vile vitongoji vinavyopakana na msitu
- v. Wajumbe wasiwe mionganii mwa wavunaji haramu wa mazao ya misitu
- vi. Wajumbe wanawake wawe angalau moja ya tatu (1/3) ya wajumbe wote.
- vii. Wajumbe wawe ni waaminifu na wenye naia ya dhati katika kutunza na kuendeleza rasilimali za msitu wa kijiji kwa manufaa jamii nzima na taifa kwa ujumla.

Baada ya kuchaguliwa na mukutano mkuu, kamati inakaa na kuchagua uongozi wake ambao ni Mwenyekiti, Katibu na Mweka Hazina kutoka mionganoni mwa wajumbe wa kamati. Kwa kipindi hiki cha mwanzo kamati hii inadumu kwa miaka mitatu na baada ya hapo itachaguliwa kamati nyingine ambayo itakuwa ya kutekeleza Mpango wa Usimamizi Shirikishi wa Misitu. Kamati hii itakuwa inadumu kwa kipindi cha miaka mitatu. Mwenyekiti wa kamati anachaguliwa kila mwaka. Kamati itakuwa inakutana kila mwezi na itakuwa inatoa taarifa kwa serikali ya kijiji kila mwezi na katika mukutano mkuu wa kijiji kila baada ya miezi mitatu.

### **2.3.2 Wajibu wa Kamati ya Maliasili ya Kijiji**

- ⇒ Kuhakikisha kwamba Msitu wa kijiji unalindwa na unatumika sawasawa na utaratibu uliowekwa kwenye Mpango wao wa Usimamizi Shirikishi wa Msitu.
- ⇒ Kufanya doria za mara kwa mara ndani ya msitu ili kuhakikisha kwamba rasilimali za msitu zinalindwa ipasavyo. Hii ni pamoja na kulimia na kufyekea mipaka ya msitu.
- ⇒ Kuwashughulikia watuhumiwa kufuatana na taratibu na sharia za Mpango wao wa Usimamizi Shirikishi wa Msitu.
- ⇒ Kuhamasisha jamii kufanya shughuli za uhifadhi wa mazingira ndani na nje ya msitu huu.
- ⇒ Kutoa taarifa za utekelezaji wa shughuli za Usimamizi Shirikishi wa Msitu kwenye serikali ya kijiji na Mkuutano mkuu wa kijiji kama ilivyoainishwa kwenye Mpango wao.
- ⇒ Kuweka kumbu kumbu za maswala yote yanayohusiana na msitu.

### **2.3.3 Wajibu wa Mwenyekiti wa Kamati ya Maliasili ya Kijiji**

- ⇒ Kuongoza vikao vyote vya kamati ya Maliasili ya Kijiji.
- ⇒ Kuhakikisha vikao vya Kamati ya Maliasili ya Kijiji vinaitishwa kulingana na Mpango wa Usimamizi Shirikishi wa Msitu na maamuzi yanatekelezwa ipasavyo.
- ⇒ Kuhakikisha taarifa za maamuzi ya kila kikao cha Kamati ya Maliasili ya Kijiji zinawafikia walengwa (serikali ya kijiji na wananchi wote kupitia mukutano mkuu wa kijiji).
- ⇒ Kuhakikisha kwamba Katibu wa Kamati ya Maliasili ya Kijiji anatunza kwa usahihi kabisa takwimu na kumbukumbu zote zinazohusiana na vikao vya ufuatiliaji wa utekelezwaji wa mpango wa Usimamizi Shirikishi wa msitu na maamuzi yaliyoafikiwa.

### **2.3.4 Wajibu wa Katibu wa Kamati ya Maliasili ya Kijiji**

- ⇒ Kuwaalika wajumbe wa Kamati ya Maliasili ya Kijiji katika vikao.
- ⇒ Kutunza vitabu vya kumbukumbu za mikutano/vikao vya kamati, kumbukumbu za doria, adhabu, faini na vibali vilivyotolewa na kamati hii.

### **2.3.5 Wajibu wa Mweka Hazina wa Kamati ya Maliasili ya Kijiji.**

- ⇒ Kutunza vitabu vyote vya fedha
- ⇒ Kutoa na kupokea fedha zote zinazohusiana na Usimamizi Shirikishi wa Msitu wao.
- ⇒ Kutoa taarifa ya mapato na matumizi ya Kamati ya Maliasili ya kijiji.

## **2.4 Taratibu za Ofisi, Usimamizi wa Fedha na Utunzaji Kumbukumbu**

### **2.4.1 Umuhimu wa Ofisi**

Viongozi ngazi ya Kijiji, Kitongoji na Mtaa wana majukumu mazito katika jamii. Ili waweze kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi wanapaswa kuelewa vema taratibu za utawala ambazo ni pamoja na uendeshaji wa ofisi na matumizi ya vifaa vilivyomo ofisini. Baadhi ya shughuli zinazofanyika maofisini ni kama zifuatazo:

- Viongozi watakutana na wananchi wenyewe kuhitaji huduma za viongozi hao;
- Vikao mbalimbali vya Kijiji, Kitongoji au Mtaa hufanyika;
- Kumbukumbu za Serikali hutunzwa;
- Mali za Serikali huhifadhiwa
- Shughuli za utawala hufanyika;
- Mawasiliano yote ya kiserikali hufanyika.

## **2.4.2 Taratibu za Ofisi**

Zifuatazo ni taratibu za ofisi kwa kifupi;

- Ofisi ni mahali mahususi pa mawasiliano. Hivyo ofisi hupokea barua za wazi na za siri, taarifa na mawasiliano ya aina yoyote. Kumbukumbu za mawasiliano hayo zinatakiwa zihifadhiwe vema katika majalada.
- Katika ofisi hutunzwa kumbukumbu za takwimu muhimu, mipango, mapato na matumizi ya kijiji, kitongoji au mtaa.
- Maamuzi yote ya Kijiji, Kitongoji au Mtaa hufanyika kwa njia ya vikao. Sheria na kanuni zinaagiza Kijiji, Kitongoji au Mtaa kuandika mihtasari ya vikao vyote.
- Nakala za mihtasari yote lazima ziwasilishwe kwenye ngazi za juu ili zikafanyiwe kazi.
- Kijiji, Kitongoji au Mtaa vinatakiwa na sheria kuwa nastakabadhi za kupokelea fedha zake na hati za malipo za kufanya malipo. Vitabu vya stakabadhi lazima visajiliwe katika rejestra na vitolewe kwa makabidhiano ya maandishi
- Utoaji wa habari ufanywe na Kiongozi aliyeidhinishwa katika ngazi ya Kijiji, Kitongoji au Mtaa, hususani Mwenyekiti.

## **2.4.3 Taratibu za Usimamizi wa Fedha**

Fedha za Serikali za Mitaa katika ngazi za Kijiji, Kitongoji na Mtaa zinapaswa kusimamiwa kwa kutumia makisio na vitabu vya mahesabu ya fedha;

### **2.4.3.1 Makisio**

Mapato na matumizi yote lazima yafanyiwe makisio ambayo yataidhinishwa na kikao cha juu cha Kijiji, Kitongoji au Mtaa kila mwaka. Katika makisio patakuwa na vipengele vifuatavyo;

### **2.4.3.2 Mapato**

#### **Mapato ya ndani**

- Mapato yatokanayo na biashara au huduma;
- Ushuru wa mazao;
- Sehemu ya mapato ya Halmashauri ya Mji au Wilaya yanayoachiwa Kijiji, Kitongoji au Mtaa;
- Ushuru na ada mbalimbali;
- Mapato mengine kwa mujibu wa sheria ndogo zilizopo; na
- Michango iliyokubaliwa na wanakijiji au wakazi wa mtaa.

#### **Mapato kutoka nje**

- Ruzuku kutoka Halmashauri;
- Mkopo kutoka taasisi za fedha;
- Msaada kutoka mashirika ya hiari;
- Misaada kutoka taasisi za maendeleo kitaifa;
- Misaada au mikopo kutoka kwa watu binafsi; na
- Mapato au mikopo kutoka vyanzo vingine.

## **2.4.4 Matumizi**

### **2.4.4.1 Matumizi ya Maendeleo**

- Huduma za jamii kama vile shule, afya, maji, kilimo na mifugo
- Huduma za uchumi na vitega uchumi, miradi ya uchumi na biashara
- Manunuzi ya mali za kudumu kama vile majengo, magari, matrekta na vifaa vya kudumu vya ofisi

### **2.4.4.2 Matumizi ya kawaida**

- Posho na mishahara
- Gharama za safari
- Gharama za ofisi
- Matumizi mengineyo yanayokubalika

#### **2.4.5 Faida za kuwa na makisio**

- Makisio yaliyoidhinishwa huwa ni idhini rasmi kutoka kwa wananchi kukusanya mapato na kutumia fedha hizo kwa ajili ya kazi zilizopangwa na kukubaliwa.
- Makisio huzuia matumizi nje ya mpango na ukusanyaji fedha kutoka kwa wananchi kiholela
- Makisio huweka mpango wa kazi za kijiji, Kitongoji au Mtaa katika kipindi cha mwaka mzima.

#### **2.4.6 Vitabu vya Mahesabu**

- Kila tendo linalohusu fedha ni lazima liandikwe kwenye vitabu vya hesabu kama mapokeo au malipo.
- Kiongozi wa Serikali ya Kijiji, Kitongoji au Mtaa anatakiwa aelewé hati muhimu za kukusanya mapato na kufanya malipo na hati za mali za Serikali zilizo katika eneo lake. Mali ya Serikali lazima iandikwe kwenye rejestra ambazo zitaelezea zilipo na chini ya uangalizi wa nani.
- Masuala yote yanayohusu malipo yafanywe kwa hati ya malipo. Mapokeo yote ya fedha yafanywe kwa stakabadhi ya Serikali. Kisha miamala yote iandikwe kama malipo au mapokeo katika daftari la fedha.

### **2.5 Kumbukumbu za Takwimu**

#### **2.5.1 Maana ya Takwimu**

Takwimu ni taarifa juu ya matukio fulani ambayo huonyeshwa kwa njia ya tarakimu, maneno au michoro ya hali halisi ya matukio hayo na sifa ambazo hazielezeki kwa njia nyingine.

#### **2.5.2 Umuhimu wa Takwimu**

Takwimu hutumika kutayarisha miradi na mipango mbalimbali ya maendeleo na kusaidia kujua ubora au udhaifu wa utekelezaji na hatua ya maendeleo iliyofikiwa. Takwimu husaidia katika kufanya maamuzi.

##### **2.5.2.1 Aina za Takwimu**

###### **Takwimu za jiografia:**

- Takwimu za maeneo na vitu vinavyopatikana katika eneo, kwa mfano eneo linalofaa kwa kilimo, ufügaji, misitu n.k.
- Takwimu za jamii: Hizi huhusiana na maendeleo na ustawi wa jamii kama vile elimu, afya na idadi ya watu.

###### **2.5.3 Umuhimu wa kutunza Rejestra:**

Ni vizuri kila aina ya takwimu katika kijiji, kitongoji au mtaa ziwe katika rejestra yake. Takwimu zihifadhiwe vema na zifanyiwe mapitio mara kwa mara iii ziende na wakati.

#### **2.5.4 Faida za kuwa na Makisio**

- Makisio yaliyoidhinishwa huwa ni idhini rasmi kutoka kwa wananchi kukusanya mapato na kutumia fedha hizo kwa ajili ya kazi zilizopangwa na kukubaliwa.
- Makisio huzuia matumizi nje ya mpango na ukusanyaji
- fedha kutoka kwa wananchi kiholela.
- Makisio huweka mpango wa kazi za kijiji, Kitongoji au
- Mtaa katika kipindi cha mwaka mzima.

# SEHEMU YA TATU

## JINSI NA JNSIA

<b>Lengo la Somo</b>	Kuelimisha viongozi katika ngazi ya kijiji na jamii kwa ujumla kuhusu dhana nzima ya Jinsi na Jinsia na mikakati ya ubereshaji iliyopo. Kufanya uchambuzi yakinifu na shirikishi ili kujua hali halisi na mikakati ya maendeleo iliyopo kijijini na jinsi ambavyo imekuwa ikiathiri wananchi kijinsia kwa lengo la kuboresha na kuweka mikakati ya pamoja ya jinsi ya kuongeza ufanisi zaidi.
----------------------	---

### 3.1 Uchambuzi wa Kijinsia katika Maendeleo

#### 3.1.1 Utangulizi

Kwa miaka mingi Serikali imeweka jitihada za kuwaendeleza wanawake kwa sababu ilidhihirika kuwa hali yao ni mbaya kuliko wanaume licha ya kuwa wanachangia sehemu kubwa ya maendeleo. Uongozi bora ni ule unaofanikisha kupatikana kwa maendeleo ya watu wote yaani wanawake na wanaume. Maendeleo ni yale yaliyozingatia usawa na mahitaji ya kijinsia ya wanawake na wanaume katika jamii. Ili kufanikisha hayo ni muhimu kwa kiongozi kuhakikisha kuwa utaratibu wa kupanga, kutekeleza, kufuatilia na kutathmini mipango ya maendeleo, unazingatia uchambuzi sio wa kijinsi tu, bali pia kijinsia.

### 3.2 Dhana ya Jinsia na Maendeleo

Jinsia inajadiliwa hapa katika mtazamo wa maendeleo. Ili kuelewa dhana hii ya jinsia na maendeleo ni muhimu kwanza kujadili maana ya jinsi na jinsia kwa sababu maneno haya yamekuwa yanatumiwa kama vile yana maana moja. **Jinsi** ni neno linalotumika kutofautisha wanawake na wanaume kimaumbile. **Jinsia** ni mahusiano ya kijamii kati ya wanawake na wanaume. Mahusiano haya yamejengwa na kuendelea kujengwa na jamii, yanaweza kubadilika kufuatana na wakati na hali ya uchumi. Haya mahusiano hujitokeza katika miundo ya kaya, mgawanyo wa majukumu, na mgawanyo wa mapato na rasilimali kama vile fedha, mali, elimu, stadi, ardhi na nyinginezo. Uchambuzi wa kijinsia unawezesha kubaini mahitaji ya msingi na yale ya kuinua hali za wanawake na wanaume katika kutekeleza majukumu yao kwa ajili ya maendeleo katika ngazi zote kuanzia ile ya kaya hadi taifa. Dhana ya jinsia na maendeleo ni mtazamo mmojawapo mpya wa kuharakisha maendeleo. Pamoja na kutambua mahitaji ya kijinsia dhana hii pia inatilia mkazo umuhimu wa kushirikiana na kutekeleza majukumu ya kijamii kwa kutegemeana kati ya wanawake na wanaume. Sera ya Maendeleo ya Wanawake ya Jinsia imezingatia dhana hii katika kuleta maendeleo ya kweli na endelevu kwa wanawake.

### 3.3 Sera ya Maendeleo ya Wanawake na Jinsia

Sera ya Maendeleo ya Wanawake na Jinsia (2000) ni mojawapo ya miongozo ya serikali unaotoa mwelekeo wa kushughulikia maendeleo ya wanawake kwa kutumia dhana ya jinsia. Sera hii inatambua kuwa maendeleo ya kiuchumi, kijamii, kisiasa na kiutamaduni ni muhimu kwa wananchi wa jinsi zote, japokuwa msukumo zaidi unahitajika kwa wanawake kwa sababu hali zao ni mbaya zaidi kuliko wanaume hapa nchini. Kwa kutambua tofauti hiyo, sera hiyo imelenga kutoa mikakati itakayoharakisha kuziba mapengo yaliyopo ya kijinsia kati ya wanawake na wanaume. Hii itakuwa ni njia mojawapo ya kutekeleza Katiba ya nchi yetu inayosisitiza usawa na heshima kwa binadamu wote, heshima ya kutambua na kuthamini utu wa mtu na haki mbele ya sheria. Kwa ujumla dhumuni kuu la sera hii ni kutoa mwelekeo utakaohakikisha kuwa mipango, mikakati na shughuli mbalimbali za uongozi na maendeleo katika kila sekta na taasisi inazingatia usawa na mahitaji ya kijinsia. Hivyo basi, utekelezaji wa sera hiyo uzingatie michango ya wahusika mbali mbali kama vile sekta za serikali na zisizo za serikali, wataalamu, watu binafsi, wanawake na wanaume. Aidha viongozi katika ngazi mbali mbali wanatakiwa kuwa chachu

na wahimizaji wakuu katika utekelezaji wake. Sera inatilia mkazo uchambuzi wa kijinsia kuwezesha uingizaji wa masuala ya jinsia katika mipango, programu na miradi ya maendeleo. Pia, Sera inahimiza kuweko kwa shughuli za maendeleo mbali mbali zinazowalenga wanawake.

### **3.4 Uchambuzi wa hali halisi ya Wanawake na Wanaume Kijinsia na baadhi ya Mikakati ya Viongozi katika ngazi ya kijiji, kitongoji na mitaa.**

Uchambuzi wa kijinsia katika masuala ya maendeleo katika ngazi zote unaonyesha kuwa wanawake wako nyuma na hali hii inahitaji kuboreshwa. Hali hiyo ya wanawake na wanaume inachambuliwa kufuatana na majukumu ya msingi ya kijamii katika uzazi na malezi; uzalishaji mali, shughuli za kujitolea katika jamii; na ushiriki katika kufanya maamuzi. Aidha, baadhi ya mikakati ya kuboresha hali hiyo kwa viongozi katika ngazi ya Vijiji, Vitongoji na Mitaa na jamii kwa ujumla pia imebainishwa katika jedwali linalojitokeza hapa chini. Utekelezaji wa mikakati hii utakuwa ni mchango wa viongozi wa kuinua hali za wanawake katika maendeleo yao na kuondoa umasikini kwa ujumla.

**Jedwali: Uchambuzi ya Hali Halisi ya Wanawake na Wanaume Kijinsia na Baadhi ya Mikakati kwa Viongozi Katika Ngazi ya Vijiji, Vitongoji na Mitaa .**

<b>Jukumu</b>	<b>Hali ya Wanawake na Wanaume Kijinsia</b>	<b>Mikakati ya Uboreshaji</b>
<b>Uzazi na Malezi:</b>  Kubeba mimba, kuzaa na shughuli zote zinazoendana na malezi, matunzo ya watoto na shughuli za nyumbani.	<p><b>Hali ikoje?</b></p> <p><b>Kimaumbile</b> wanawake wana husika na kubeba mimba, kuzaa na kunyonyesha.</p> <p><b>Kijinsia</b> wanawake hufanya shughuli zote zinazoendana na malezi, matunzo ya watoto, baba na wana familia wengine. Aidha, hufanya shughuli za nyumbani kama vile kutayarisha na kupika chakula, kutafuta kuni, maji usafi wa nyumbani na mazingira yake n.k.</p> <p><b>Wanaume</b> kwa upande wao hujishughulisha kwa kiasi kidogo katika masuala ya uzazi na malezi.</p> <p>Aidha shughuli nyingine ni za msimu kama vile ujenzi wa makazi, usafi wa mazingira na kuhudumia wagonjwa na wazee ikibidi.</p> <p><b>Matatizo kwa wanawake:-</b> Vifo vingi nya uzazi (wanawake 530 kwa kila wanawake 100,000) hufa kwa sababu wengi huzaa watoto wengi, baadhi huzaa katika umri mdogo, kushindwa kumudu gharama za afya, matatizo yatokanayo na kukeketwa, huduma zisizotosheleza za afya na uzazi wa mpango,</p>	<ul style="list-style-type: none"> <li><input type="checkbox"/> Kuhamasisha kuacha mila na desturi potofu kama vile kukeketa wanawake.</li> <li><input type="checkbox"/> Kuhamasisha wanawake na wanaume kupanga uzazi kulingana na uwezo wao wa kuwatunza na kuwaendeleza; kutoa muda wa kutosha kwa wanawake kunyonyesha, kupumzika na kushiriki katika maendeleo yake na ya kijamii vizuri zaidi</li> <li><input type="checkbox"/> Kuboresha njia za mawasiliano ikiwa ni pamoja na barabara za vijijini, kuwezesha upatikanaji wa huduma za afya kwa wanawake kwa haraka na urahisi.</li> <li><input type="checkbox"/> Kuhimiza matumizi ya teknolojia sahihi kama vile mikokoteni, majiko sanifu kwa lengola kupunguza mzigو wa kazi na kuhifadhi mazingira.</li> <li><input type="checkbox"/> Kusimamia hifadhi ya mazingira, ardhi, vyanzo nya maji, kuhimiza ujenzi na matumizi ya vyoo na mifereji ya maji taka.</li> <li><input type="checkbox"/> Kusimamia utekelezaji wa sera na sheria zenye malengo ya kutokomeza vitendo nya ukatili, ubaguzi.</li> </ul>

<b>Jukumu</b>	<b>Hali ya Wanawake na Wanaume Kijinsia</b>	<b>Mikakati ya Uboreshaji</b>
	<p>kutembea masafa marefu kupata huduma za afya, maji, kuni n.k.; lishe duni; kukabiliwa na uambukizo na mzigo wa kutunza walioathirika na UKIMWI; na hutumia muda mwingu (saa 16-18 kwa siku) kwa malezi, utunzaji wa nyumbani na uzalishaji mali wakibakiwa na muda mdogo wa kupumzika.</p>	<ul style="list-style-type: none"> <li><input type="checkbox"/> Unyanyasaji wa kijinsia. Baadhi ya sheria na Sheria ya Makosa ya Jinai ya kujamiana (1998); na Sheria ya Ardhi na Ardhi Vijijini (1999).</li> <li><input type="checkbox"/> Kuhimiza uanzishaji wa vituo vyta kulelea watoto kwa lengo la kuwapunguzia wanawake mzigo wa kazi.</li> <li><input type="checkbox"/> Kuhimiza jamii na kusimamia uzalishaji na kuhifadhi chakula cha kutosha na kuuza ziada tu.</li> <li><input type="checkbox"/> Kuhamasisha jamii ili wanawake na wanaume waweze kushiriki katika kufanya kazi zote kulingana na uwemo wao ambazo zinafanywa na wanawake.</li> <li><input type="checkbox"/> Kujadili suala la UKIMWI kwa uwazi katika ngazi ya jamii na vikao mbali mbali ili kupata ufumbuzi wenye mtazamo wa kijamii wa kubadili tabia kuhusu ngono, matunzo kwa walioathirika, watoto yatima na mengineyo.</li> </ul>
<b>Uzalishaji mali:</b>  Kazi za ujira wa fedha au mali.	<p><b>Hali ikoje vijijini? Wanawake</b> wengi takribani 90% ni wazalishaji katika sekta ya kilimo cha chakula na biashara. Wanatumia saa 3 - 4 zaidi katika shughuli za kulima, kupanda, kupalilia na kuvuna kuliko wanaume.</p> <p><b>Wanaume</b> wana jishughulisha zaidi na mazao ya biashara na wana mamlaka zaidi juu ya matumizi ya mapato yatokanayo na kilimo katika ngazi ya kaya kuliko wanawake.</p> <p><b>Matatizo kwa wanawake:</b></p> <ul style="list-style-type: none"> <li><input type="checkbox"/> Wanatumia teknolojia ya kale kama vile majembe ya mkono nguvu kazi hafifu n.k.</li> <li><input type="checkbox"/> Ujuzi mdogo kwa kuwa huduma za ugani haziwafikii waliorwengi</li> <li><input type="checkbox"/> Hawana mamlaka juu ya mapato wanayozalisha.</li> </ul>	<ul style="list-style-type: none"> <li><input type="checkbox"/> Kuhimiza uboreshaji wa kilimo kwa wanawake na wanaume kwa lengo la kuongeza uzalishaji kwa kutumia pembejeo na vitendea kazi bora ikiwepo mbolea za asili.</li> <li><input type="checkbox"/> Kuhimiza matumizi bora ya pamoja (wanawake na wanaume) ya mapato yatokanayo na kilimo.</li> <li><input type="checkbox"/> Kuimarisha upatikanaji wa mitaji ya kuendeshea miradi ya uzalishaji mali kama vile mikopo na vyama vyta kuweka na kukopa.</li> <li><input type="checkbox"/> Kuhamasisha uanzishwaji wa vyama vyta kuweka na kukopa kwa akina mama ili waweze kupata mitaji ya kuendeshea miradi yao.</li> <li><input type="checkbox"/> Kuhimiza halmashauri kuongeza viwango vyta kuchangia mifuko ya Maendeleo ya wanawake ili walio wengi waweze kupata mikopo itakayowawezesha kujiimarisha kiuchumi. Aidha kuhimiza urejeshwaji wa mikopo na kwa wakati ili waweze kuwakopesha wanawake walio wengi zaidi.</li> </ul>

Jukumu	Hali ya Wanawake na Wanaume Kijinsia	Mikakati ya Uboreshaji
	<p><b>Hali ikoje Mjini?</b></p> <p>Wanawake wengi takribani 44.1% ni wazalishaji mali katika sekta isiyo rasmi. Wanafanya biashara ndogo ndogo yenye mapato kidogo kama vile kuza chakula “mama ntilie”, ususi, kugonga kokoto, kuza mkaa na nyiningezo. Katika sekta isiyo rasmi, wanaume wengi wamewekeza katika miradi yenye mapato ya wastani au ya juu ikilinganishwa na wanawake.</p> <p><b>Matatizo kwa wanawake:-</b></p> <p>Upungufu wa mitaji, masoko, nyenzo, utaalamu, ujuzi, na maeneo ya kufanya biashara.</p> <p><b>Katika ajira rasmi wanawake</b></p> <p>wanaopata ajira ni wachache sana (takriban 32%) wengi wao wakipata ajira katika nafasi za ngazi ya chini zenye ujira mdogo.</p> <p><b>Katika ajira rasmi wanaume</b> wako kwenye nafasi za kati na za uongozi zenye ujira mzuri.</p> <p><b>Matatizo:</b></p> <p>Elimu duni kwa wanawake. Ni kweli kwamba kuna watoto wengi wa kike ambao hawaandikishwi shule, hata wale walioandikishwa hawafaulu vizuri kama wavulana kwa sababu ya kukosa muda mzuri wa kujisomea nyumbani kwa ajili ya kufanya kazi za kusaidia uzalishaji mali, malezi na shughuli za nyumbani; Wengi hawamalizi shule kotokana na kupata ujauzito, na wengine kutokulipiwa ada za shule.</p> <p>Aidha watoto wa kike wameonekana kutochukua fani za masomo ya sayansi, hisabati, ufundu na teknolojia ambayo yangewawezesha kupata ajira zenye ujira mkubwa.</p>	<ul style="list-style-type: none"> <li><input type="checkbox"/> Kuhimiza wanawake na wasichana wengi ili waweze kuijunga na mafunzo ya ufundu na utaalamu mbalimbali ili waweze kupata ujuzi na stadi.</li> <li><input type="checkbox"/> Kuhamasisha wanawake na wanaume wengi ili waweze kuwekeza katika nyenzo bora ili kuongeza uzalishaji mali.</li> <li><input type="checkbox"/> Kuweka utaratibu maalumu (wenye urasimu mdogo) wa kutoa leseni kwa wafanya biashara ndogo ndogo.</li> <li><input type="checkbox"/> Kuwaelimisha wazazi na jamii kwa ujumla ili waweze kutoa nafasi sawa za masomo kwa wavulana na wasichana. Fursa sawa za kupata elimu, kusaidia kazi za nyumbani, na kujisomea nyumbani baada ya kutoka shule.</li> <li><input type="checkbox"/> Kuhamasisha jamii pamoja na mashirika yasiyo ya kiserikali kushiriki katika ujenzi na ukarabati wa shule na mabweni ya wasichana ili kuongeza idadi yao na pia kuwalinda dhidi ya athari zinazoweza kuwakatisha masomo, na kuwawezesha kupata muda wa kujisomea.</li> <li><input type="checkbox"/> Kuwahamasisha wanawake na wasichana kuijunga na masomo ya sayansi, vyuo vya juu na vyuo vikuu ili wapate elimu ya juu na utaalamu wa kutosha kwa ajili ya kupata ajira nzuri na ujira bora zaidi (au kujiajiri).</li> </ul>

<b>Jukumu</b>	<b>Hali ya Wanawake na Wanaume Kijinsia</b>	<b>Mikakati ya Uboreshaji</b>
<b>Shughuli za jamii za kujitolea:</b> Kuchangia nguvu kazi, fedha au mali ili kupata huduma au mali kwa ajili ya matumizi ya jamii	<p><b>Hali ikoje?</b></p> <p><b>Wanawake</b> wameonekana kuchangia nguvu kazi, fedha au mali katika upatikanaji na utunzaji wa vifaa vya huduma kama vile ujenzi wa shule, vituo vya afya, maji kwa ajili ya matumizi ya wengi n.k.</p> <p><b>Wanaume</b> wameonekana katika kuchangia upatikanaji wake kuliko utunzaji.</p> <p><b>Matatizo kwa wanawake</b></p> <p>Pamoja na kuwa shughuli hizi za kujitolea ni muhimu, kwa wanawake huongezea mzigo wa kazi hasa katika suala la kuchangia nguvu kazi na utunzaji hasa ikizingatiwa mzigo mkubwa wa kazi walio nao.</p>	<ul style="list-style-type: none"> <li><input type="checkbox"/> Kuhimiza jamii kuchangia katika miradi itakayowezesha kuwapunguzia wanawake mzigo wa kazi kama vile kuanzisha vituo vya kulelea watoto.</li> <li><input type="checkbox"/> Kuhamasisha wanaume kuchangia zaidi nguvu kazi na kujihusisha na utunzaji wa vifaa na huduma zilizopatikana kwa njia ya kujitolea kwa lengo la kuzidumisha na kuwapunguzia mzigo wanawake.</li> <li><input type="checkbox"/> Kuwashirikisha wanawake na wanaume katika kupanga muda muafaka wa kuchangia nguvu kazi katika shughuli za kujitolea.</li> </ul>
<b>Kufanya maamuzi na kushiriki katika siasa</b>  Hii ni njia ya ushiriki ambayo inahakikisha kuwa mahitaji ya kijinsia yaliyobainishwa na wanawake na wanaume yanawekwa bayana katika sera, mpango miradi na shughuli za maendeleo na utekelezaji wake kuanzia ngazi ya Kaya mpaka Mtaa	<p><b>Hali ikoje?</b></p> <p>Wanawake hawashiriki katika maamuzi kwa kiasi cha kutosha katika masuala ya maendeleo katika ngazi ya kaya hata yale yanayowahusu kama vile kuchaguliwa masomo, waume, kukeketwa na mengineo.</p> <p><b>Wanawake</b> ni wachache katika uongozi wa Vijiji, vitongoji, Mitaa na hata vyombo vya uwakilishi. Hii imesababisha kuwepo na viti maalum vya uwakilishi katika Bunge (20%) na Serikali za Vijiji, Halmashauri za Wilaya, Miji, Manispaa na Jiji kuwa 33.3%).</p> <p><b>Wanaume</b> wameonekana kushika nafasi nyingi za uongozi na uwakilishi.</p> <p><b>Matatizo</b> - wanawake wachache tu hujitokeza katika kugombea nafasi za uongozi na uwakilishi, hawana mbinu za kisiasa. Kutojiamini, jamii kutothamini uongozi wa wanawake na wengi kukosa elimu ya kutosha.</p>	<ul style="list-style-type: none"> <li><input type="checkbox"/> Wanawake wapewe nafasi ya kutoa mchango wao katika vikao, vyombo vya maamuzi na uwakilishi. Aidha wapewe nafasi ya kubaini, kupanga, kutekeleza na kutathmini mipango, programu na miradi ya maendeleo katika ngazi mbalimbali kwa ajili ya kuhakikisha kuwa mahitaji yao ya kijinsia yanazingatiwa, mkakati huu unaimarisha utawala na uongozi bora.</li> <li><input type="checkbox"/> Kuwashawishi wanawake kujitokeza katika kugombea nafasi za uongozi na uwakilishi.</li> <li><input type="checkbox"/> Na mikakati mingine iliyotolewa hapo juu kama vile ya kuimarisha elimu ya wanawake na wasichana, kuimarisha uzalishaji mali iii kuongeza uwezo wao wa kujiamini.</li> </ul>

### **3.5 Jinsi ya kuweka usawa wa kijinsia katika ngazi ya Kijiji**

- a. Kijiji kitoe haki sawa ya uanachama kwa jinsia zote.
- b. Kamati za vijiji ziundwe na uwiano ulio sawa wa wanawake na wanaume.
- c. Vikundi vyote vya miradi ya maendeleo itakayoanzishwa hapa kijijini viundwe kwa uwiano sawa wa wanawake na wanaume.
- d. Mipango ya miradi ijumuushe matatizo ya wanawake yanayotokana na uchambuzi wao wenyewe.
- e. Mipango yote katika mpango wa kuboresha jamii lazima inufaishe wanawake na wanaume.
- f. Shughuli ngumu zitakazopangwa na zizingatie majukumu anayofanya mwanamke, na hali anayokuwa nayo, k.m. ujauzito, au kujifungua karibuni. Hivyo utaratibu unaweza kuwekwa ili mwanamke wa hali kama hii aweze kusamehewa au kupewa kazi rahisi ili asinyimwe haki yake.
- g. Uongozi wa kijiji ushirikiane na jamii nzima kupiga vita mila na imani potofu zinazogandamiza wanawake.
- h. Uongozi wa kijiji utoe haki sawa kati ya wanawake na wanaume hasa wakati wa kuchangia mijadala mbali mbali inayohusu maendeleo ya kijiji.





